


The United Republic of Tanzania



Ministry of Health

National TB and Leprosy Programme

# TB05 - TB LAB REGISTER

**REGION** \_\_\_\_\_ **COUNCIL** \_\_\_\_\_ **FACILITY** \_\_\_\_\_

**Laboratory Register: TB 05**

Rejista hii inajazwa taarifa za wahisiwa wa ugonjwa wa Kifua Kikuu na wagonjwa waliopo kwenye matibabu pamoja na matokeo ya vipimo vya sampuli (sputum/stool/Urine n.k) kwa ajili ya ugunduzi na ufuatiliaji wa Kifua Kikuu. Rejista hii inajazwa na watoa huduma za afya wa maabara walioko katika vituo tiba/uchunguzi wa Kifua Kikuu (diagnostic centres). Taarifa za mwanzo/kuomba upimaji zinatolewa kwenye fomu ya "Request and report form for biological specimen for TB and Leprosy" (TB/LEP 01).

**Hakikisha sehemu zote zinajazwa ipasavyo. NAMNA YA UJAZAJI**

Andika mwaka katika kila ukurasa mpya unaoanza kujaza.

**Safu ya (1) Lab serial number:** Andika namba mtiririko ukianza na namba 1 unapoanza mwaka mpya.

**Safu ya (2) Date Sample collected/Date of examination:** Jaza juu tarehe ambayo sampuli ilichukuliwa, na chini jaza tarehe ambayo kipimo kimefanyika (siku, mwezi na mwaka).

**Safu ya (3) Full name:** Andika majina halisi matatu ya mgonjwa (Jina la kwanza, Kati na Ukoo).

**Safu ya (4) Sex:** Jaza **F** kama mgonjwa ni mwanamke na **M** kama mgonjwa ni mwanaume.

**Safu ya (5) Age:** Jaza miaka kamili ya umri wa mgonjwa. Iwapo ana umri chini ya mwaka mmoja Andika sifuri (0).

**Safu ya (6) Physical address/Telephone number:** Jaza mahali anapoishi kwa sasa (Kitongoji/mtaa, Kijiji/mji, kata, namba ya nyumba) na namba ya simu ya mgonjwa (Mahali anapoishi kwa sasa "Physical address" juu na Namba ya Simu ya Mteja/Mgonjwa kwa "Telephone number" chini)

**Safu ya (7) Name of area leader:** Andika jina la mwenyekiti wa serikali ya Mtaa/Kitongoji/Jirani.

**Safu ya (8) Name of referring health facility clinic/ward:** Andika jina la kituo, kliniki au wodi iliyompa rufaa mgonjwa kuomba upimaji wa kipimo.

**Safu ya (9) HIV status:** Andika hali ya VVU ya mgonjwa (Pos; Neg; Unkn).

**Safu ya (10) Specimen type:** Andika namba ya aina ya sampuli kutoka kwenye kielelezo \*\*\*(sputum, stool, urine, etc). Ikiwa aina ya Sampuli ni "Other", Taja

**Safu ya (11) Date/Time in:** Andika tarehe na saa ambayo sampuli ilipokelewa maabara (tarehe juu na saa chini)

**Safu ya (12) Date/Time out:** Andika tarehe na saa ambayo majibu yalitoka maabara (tarehe juu na saa chini)

**Safu ya (13) Diagnosis:** Weka alama ya vema (√) iwapo mgonjwa anapima kipimo kwa ajili ya ugunduzi wa Kifua Kikuu.

**Safu ya (14) GeneXpert result:** Jaza matokeo ya kipimo cha GeneXpert (RR kama ni MTB+/RIF+, T kama ni MTB+/RIF-, N kama ni MTB-, Ti kama ni MTB detected Rifampicin resistance indeterminate, TT kama ni MTB detected trace, Rifampicin resistance indeterminate, I kama ni Invalid, Error au No result).

**Safu ya (15) Truenat result:** Jaza matokeo ya kipimo cha Truenat (RR kama ni MTB+/RIF+, T kama ni MTB+/RIF-, N kama ni MTB-, Ti kama ni MTB detected Rifampicin resistance indeterminate, I kama ni Invalid, Error au No result).

**Safu ya (16) TB LF-LAM:** Jaza matokeo ya kipimo cha TB LF-LAM (Neg, Pos, Indeterminate, Invalid)

**Safu ya (17) Smear Microscopy result:**

- Jaza matokeo ya kipimo che smear microscope (Neg, Scanty, 1+, 2+, 3+) kwenye safu husika kulingana na muda sampuli ya makohozi ilipotolewa. (Safu A iwapo ni sampuli ya "Spot" (papo kwa papo) na B kama ni ya "morning" (asubuhi).
- Jaza idadi kamili ya "AFB" (Vimelea) iwapo matokeo ni scanty.
- Jaza kwa kutumia kalamu ya wino mwekundu iwapo matokeo ni Positive (Scanty, 1+, 2+, 3+).

**Safu ya (18) Follow up:** Weka alama ya vema (√) chini ya safu husika ya mwezi wa upimaji makohozi ya ufuatiliaji.

**Safu ya (19) Specimen referred to:** Andika jina la maabara ambayo sampuli imeenda kupimwa kwa molecular (GeneXpert Site au Truenat Site) baada ya kupima na microscope.

**Safu ya (20) Name of laboratory staff:** Andika jina la mtaalamu wa maabara aliyefanya kipimo hicho (majina mawili).

**Safu ya (21) TB Registration Number:** Andika na namba ya usajili ya mgonjwa wa Kifua Kikuu kutoka rejesta TB 03.

- Namba ya usajili ya mgonjwa ijazwe kwa kalamu ya wino mwekundu kwa wagonjwa wote waliogundulika kuwa na vimelea ya Kifua Kikuu (smear positive).
- Kwa wagonjwa wa kipimo cha makohozi ya ufuatiliaji, jaza namba ya usajili kwa kalamu ya wino wa blue.

**Safu ya (22) Remarks:** Andika maoni au maelezo mengine muhimu yanayomhusu mgonjwa au kipimo.



